



TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA  
Kitalu Na. 339, Mtaa wa Nyerere - Kilimani  
S.L.P 4019, DODOMA  
Simu: +255 22 2135747/8; 2137125; 2135222  
Faksi: +255 22 2111281  
Barua Pepe: [info@chragg.go.tz](mailto:info@chragg.go.tz)  
Tovuti: [www.chragg.go.tz](http://www.chragg.go.tz)

Novemba 21, 2019

## **TAARIFA KWA UMMA**

### **THBUB kufuatilia uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2019**

Kama tunavyofahamu kuwa siku ya Jumapili Novemba 24, 2019 Watanzania kote nchini watafanya uchaguzi wa viongozi ngazi ya Serikali za Mitaa. Hatua hiyo ya uchaguzi imetanguliwa na uandikishaji wapiga kura, uteuzi wa wagombea na kampeni za wagombea, hatua ambazo zimetetekezwa kwa mafanikio makubwa.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeridhishwa na idadi ya watu waliojitokeza kujiandikisha kupiga kura. Idadi hiyo imeongezeka ukilinganisha na idadi ya watu waliojiandikisha katika uchaguzi kama huo uliofanyika mwaka 2014.

Katika kipindi kama hiki cha uchaguzi zipo taasisi za ndani na nje ya nchi ambazo zimeteuliwa kama waangalizi wa uchaguzi kwa mujibu wa Sheria ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288.

Napenda kuujulisha umma wa Watanzania kuwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni mojawapo ya taasisi ambayo itafanya ufuatiliaji wa uzingatiwaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora wakati wa uchaguzi na baada

